HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOMBE

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOMBE KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 KUISHIA TAREHE 31 OKTOBA, 2020

1.0 UTANGULIZI

Mhe. Mkuu wa Mkoa;

Wilaya ya Bukombe ipo kati ya Latitude 3˚00’ na 4˚30’ Kusini mwa Ikweta. Wilaya ina ukubwa wa eneo la km² 8,055.59 sawa na asilimia 20.6% ya eneo lote la Mkoa wa Geita. Eneo la ukubwa wa km² 1,766.59 sawa na asilimia 22% ya eneo lote la Wilaya linafaa kwa kilimo, ufugaji na makazi. Eneo la hifadhi ni km² 6,289 sawa na asilima 78% ya eneo lote la Wilaya ya Bukombe. Hali ya Hewa ya Wilaya ni ya Ki – Tropiki yenye wastani wa joto 22˚C na wastani wa mvua kwa mwaka ni kati ya 900mm – 1200mm.

2.0 IDADI YA WATU

Mhe. Mkuu wa Mkoa;

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, Wilaya ya Bukombe ina jumla ya watu 224,542, wanawake wakiwa ni 113,685 na wanaume 110,857. Kiwango cha ongezeko la watu ni 5.9%. Hivi sasa Wilaya inakadiriwa kuwa na watu 301,403. Ongezeko hilo linachangiwa na kuzaana (55%) na uhamiaji (45%). Wastani wa ukubwa wa kaya ni watu 6. Msongamano wa watu katika eneo la makazi (Population Density) ni watu 27 kwa km². Wilaya hii ina watu 142,890 wenye uwezo wa kufanya kazi (nguvu kazi) yaani miaka 15 - 64, sawa na asilimia 47.7 ya idadi ya watu wote kwa sasa.

JEDWALI Na. 01: MCHANGANUO WA IDADI YA WATU KIKATA

Na;	KATA	WANAUME	WANAWAKE	JUMLA
1	Bugelenga	5,566	5,794	11,360
2	Bukombe	7,699	8,014	15,713
3	Busonzo	6,772	7,048	13,820
4	Butinzya	6,496	6,762	13,258
5	Bulega	8,892	9,255	18,148
6	Igulwa	10,871	11,315	22,186
7	Iyogelo	5,203	5,415	10,618
8	Lyambamgongo	4,153	4,322	8,475
9	Namonge	20,162	20,985	41,147
10	Ng'anzo	5,868	6,108	11,976
11	Runzewe Magharibi	7,886	8,208	16,094
12	Runzewe Mashariki	10,586	11,018	21,604
13	Ushirombo	3,973	4,135	8,107
14	Uyovu	19,672	20,475	40,147
15	Katome	5,413	5,634	11,047
16	Katente	13,143	13,679	26,822
17	Bulangwa	5,332	5,549	10,881
JUMLA		**147,687**	**153,716**	**301,403**

Chanzo: Ofisi ya Takwimu ya Taifa, 2017

3.0 HALI YA UTAWALA

Mhe. Mkuu wa Mkoa;

Ki-utawala Halmashauri ya Wilaya ina Tarafa 3, Kata 17, vijiji 64 na vitongoji 348. Wilaya hii ina Jumla ya Shule za Msingi 86 (Shule 80 zinamilikiwa na Serikali Shule 06 zinamilikiwa na mtu binafsi), Shule za Sekondari 18 (Shule 15 zinamilikiwa na Serikali na Shule 03 zinamilikiwa na watu binafsi).

Pia Wilaya inajumla ya vituo vya tiba 18 vinavyofanya kazi, ambavyo ni hospitali moja ya serikali; Vituo vya afya 5 kati ya hivyo, 3 ni vya Serikali na 2 ni vya binafsi; zahanati 11, kati ya hizo 7 ni za serikali na 4 ni za binafsi; na kliniki 1 inayotoa huduma za Afya ya uzazi tu (Martenity home)

4.0 USIMAMIZI WA FEDHA

Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe inasimamia fedha kwa kutumia mifumo ifuatayo mbalimbali ambayo imewekwa na TAMISEMI. Mifumo hiyo ambayo inasimamia fedha nikama ifuatavyo;

i. Mfumo wa mapato wa LGRCIS,
ii. Mfumo funganishi wa Epicor
iii. Mfumo wa FFAS
iv. Mfumo wa Hospital wa GOTMIS.

Halmashauri ya wilaya ya Bukombe in jumla ya POS 95 ambazo 43 tulipata mgao kutoka kwa Waziri wa TAMISEMI na POS 52 Halmashauri ilinunua kwa mapato yake ya ndani aidha POS zinazotumika ni 45 na zingine zipo stong room.

5.0 TAARIFA YA MAPATO YA NDANI

5.1 Makusanyo ya Mapato ya Ndani

Halmashauri ilipanga kukusanya jumla ya **Tshs. 1,456,548,000.00** (kila mwezi kiasi cha **Tshs. 121,379,000.00**) kutoka kwenye vyanzo vyake vya ndani ya Mfumo. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai hadi kuishia 31 Oktoba, 2020 Halmashauri imefanikiwa kukusanya kiasi cha **Tshs. 329,307,549.22** ikiwa ni sawa na asilimia **22.61**

Kwa mpango kazi wa Mkausanyo ya Mapato ya Ndani hadi kufikia Mwezi Oktoba Halmashauri ya Wilaya ilitakiwa iwe imekusanya kiasi cha **Tshs. 485,516,000.00** na kwa makusanyo yaliyokusanywa ni pungufu kwa kiasi cha **Tshs. 156,208,450.78** sawa na asilimia **32.17**

5.2 CHANGAMOTO ZA UKUSANYAJI WA MAPATO

Ukusanyaji wa mapato kwa Kutumia Mawakala

Halmashauri ya wilaya ya bukombe imekuwa ikikusanya mapato yake ya ndani kwa kutumia mawakala wa kukusanya mapato yake ya ndani na kuanzia mwezi oktoba baadhi ya vyanzo vimepewa watumishi ili waweze kukusanya mapato hayo vyanzo hivyo ni;

i. **Maegesho ya magari Ushirombo** ambayo wakala alikuwa anakusanya wastani wa million mbili kwa mwezi na sasa mtumishi amekusanya 4,026,000/ kwa mwezi wa oktoba peke yake
ii. **Maegesho ya Uyovu** ambayo wakala alikuwa anakusanya wastani wa million moja kwa mwezi na mtumishi amekusanya jumla ya Tshs 3,100,000 kwa mwezi.

iii. **Ushuru wa mbuzi soko la ibamba** wakala alikuwa anakusanya watini wa 480,000 na mtumishi amekusanya Tshs 1,200,000 kwa mwezi oktoba

iv. **Mnada wa Mifugo Bukombe** na **Mnada wa Mifugo Busonzo** zote zinakusanywa na watumishi kwa sasa ambapo mapato kwa mwezi wa oktoba pekee zimekusanywa jumla ya **Tshs 21,911,500.**Tofauti na mawakala ambapo kwa mwezi Julai pekee mawakala walikusanya jumla ya **Tshs 17,593,000**

v. **Ushuru wa mazao ya Misitu** Kumekuweko na mkanganyo ya namna ya ukusanyaji wa tozo mbali mbali za ushuru wa mazao ya misitu kwa Halmashauri ya wilaya ya Bukombe na wakala wa Misitu Tanzania (TFS) ambapo tozo hizo TFS wamekuwa wakikusanya huku halmashauri ikikosa ushuru huo ambao ndo chanzo cha mapato kikuu kwa Halmashauri ya wilaya ya Bukombe ambapo kwa miaka ya nyuma halmashauri imekuwa ikikusanya mapato hayo changamoto hii bado haijatatuliwa pamoja na kukaa vikao kwa pande zote mbili na ofisi ya mkuu wa wilayaya Bukombe na Meneja wa TFS kanda.

5.3 MIKAKATI YA KUBORESHA UKUSANYAJI WA MAPATO.

Kamati ya Mapato ilikagua vyanzo vya mapato ya ndani ya Halmashauri kuona fursa na changamoto zinazopunguza ufanisi katika shughuli za ukausanyaji wa mapato hayo. Baada ya hapo ilitoa mapendekezo ili kuboresha mazingira ya ukusanyaji na usimamaizi wa mapato.

i. **SOKO LA LYOBAHIKA**

- Kulikuwa na changamoto ya kutokusanywa mapato ya Halmashauri kwenye eneo la soko la Lyobahika Mabatini kata ya Uyovu ambapo kamati ilipendekeza yafuatayo:-
- Kujenga choo cha kisasa kwa ajili stendi na soko hilo ili kuongeza mapato ya Halmashauri.
- Mtendaji wa Kijiji cha Lyobahika aliteuliwa kuwa Afisa Masoko atakaesimamaia shughuli zote za Soko hilo.
- Halmashauri inatarajia kukusanya mapato kutoka kwenye meza za soko la Lyobahika jumla ya Tsh.360 * 5,000=1,800,000 kwa mwezi na mapato ya vibanda 348*10,000 sawa na Tshs 3,480,000 kwa mwezi.

ii. **SOKO LA KILIMAHEWA**

Halmashari ya wilaya bukombe imefanya mkakati wa kuboresha mapato yake ya ndani kwa kupanga mkakati wa ujenzi wa soko la kilimahewa kata ya bulangwa ilikuongeza mapato yake ya ndani**.**

- Kamati ya Mapato ya wilaya ya Bukombe ilipendekeza ufanyike usanifu wa vibanda 81 na kila kibanda kipewe namba ii kuvitambua ambapo wafanyabiashara watajenga vibanda hivyo kwa gharama zao kwa mikataba ya miaka mitano ambapo halmashauri itakuwa inalipwa pango la Tshs 10,000/ kwa kila kibanda kwa kwezi hii itaongeza mapato yake ya ndani.
- Halmashauri inategemea kutanga ugawaji wa viwanja kwa ajili ya ujenzi wa vibanda hivyo mwezi huu wa novemba 2020 ili wafanyabishara wanaohitaji kujenga vibanda kuzunguka soko hilo watume maombi.

iii. **USHURU WA VIBANDA VINAVYO ZUNGUKA SOKO NA STENDI KUU YA MABASI USHIROMBO.**

Halmashauri ya wilaya ya Bukombe imewaandikia barua wapangaji wa vibanda vinavyo zunguka soko kuu na stendi kuu ya mabasi Ushirombo ikiwataka kuanza kulipa ushuru wa vibanda wa Tshs 10,000 kwa mwezi kwa mujibu wa sheria ndogo za Halmashauri badala ya Tshs 5,000 kwa mwezi Kuanzia julai 2020.ambapo itaongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri.

5.4 Muhutasari wa Mapato na Matumizi ya Bajeti kwa Mwaka 2020/2021

Matumizi na Mapato ya Halmashauri kuanzia Julai hadi Oktoba, 2020 ni kama ifuatavyo;

Jedwali Na: 02 Mapato na Matumizi kwa Julai hadi Oktoba, 2020

CHANZO	MAKISIO YA BAJETI 2020/2021	MAPATO HALISI KWA MWEZI OKTOBA	%	MATUMIZI KWA MWEZI OKTOBA	%
Mishahara ya Watumishi	60,069,718,998.00	6,467,664,760.00	10.77%	4,782,569,160.00	73.95%
Miradi ya Maendeleo – Wahisani	6,979,504,293.00	947,659,124.11	13.58%	923,830,338.08	97.49%
Matumizi mengineyo - OC	1,354,144,000.00	564,379,500.00	41.68%	220,376,716.74	39.05%
Mapato ya ndani	1,945,991,292.00	410,184,937.95	21.08%	278,807,277.34	67.97%
Nje ya Mfumo	489,443,292.00	80,877,388.73	16.52%		
Ndani ya Mfumo	1,456,548,000.00	329,307,549.22	22.61%		
JUMLA	**70,349,358,583.00**	**8,389,888,322.06**	**11.93%**	**6,205,583,492.16**	**73.97%**

Chanzo: Idara ya Fedha

5.5 Mchango wa Halmashauri kwenye Miradi ya Maendeleo kwa kupitia Mapato ya Ndani

Jedwali Na. 03: Asilimia 40 ya Miradi ya Maendeleo

MAKISIO YA BAJETI 2020/2021	KIASI CHANGIWA JULAI HADI OKTOBA, 2020	%
582,619,200.00	100,066,884.81	17.18%

5.6 Mchango wa Halmashauri kwa ajili ya vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu

Jedwali Na. 04: Asilimia 20 ya Vikundi kwa mwaka wa fedha 2020/2021

MAKISIO YA BAJETI 2020/2021	KIASI KILICHOCHANGIWA JULAI HADI OKTOBA, 2020	%	KIASI KILICHOKOPESHWA	%
143,154,800.00	36,437,476.77	25.45%	28,100,000.00	77.12%

(*Mchanganuo wa Miradi ya Maendeleo na Vikundi vilivyokopeshwa kupitia Mapato ya Ndani umeambatishwa katika Majedwali*)

6.0 MAPOKEZI YA FEDHA ZA MIRADI ZA MAENDELEO

Mhe. Mkuu wa Mkoa;

Katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Halmashauri kwa Mwaka wa Fedha **2020/2021,** Halmashauri ilipanga kutumia kiasi cha **Tshs. 6,949,711,750.98** kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za Miradi ya Maendeleo katika Sekta Mbalimbali. Fedha hizo zilipaswa kutoka katika vyanzo vikuu 4 ambavyo ni Mapato ya ndani, Ruzuku toka Serikali Kuu, Wafadhili na Jitihada za Jamii.

Mhe. Mkuu wa Mkoa;

Hali ya upatikanaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo hadi kufikia tarehe 31 Oktoba, 2020 si wa kuridhisha, Halmashauri imepokea kiasi cha Tshs. **947,659,124.11** sawa na asilimia **13.6** ya fedha zilizopangwa kwa Mwaka Mzima ambazo ni **Tshs. 6,949,711,750.98** Fedha hizi zilizopokelewa zimetoka katika vyanzo mbalimbali (**TASAF, MDH, Global Fund, Elimu Bure Msingi na Sekondari n.k**)

Hadi kufikia tarehe 31 Oktoba, 2020 kiasi cha **Tshs. 923,830,338.08** kilikuwa kimeshatumika sawa na asilimia **97.49** ya fedha iliyotolewa katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo kama **Jedwali Na; 05** linavoonyesha hapo chini.

Jedwali Na 05: Muhtasari wa Mapokezi na Matumizi ya Fedha za Maendeleo kuishia 30 Oktoba, 2020

Na	CHANZO CHA FEDHA	FEDHA PANGWA	FEDHA TOLEWA		FEDHA TUMIKA	
			KIASI	%	KIASI	%
1	Serikali Kuu (MSD)	571,735,811.00	-	-	-	-
2	Mfuko wa Pamoja wa Afya (HSBF)	670,274,000.00	-	-	-	-
3	Malipo kwa Ufanisi (RBF)	938,394,000.00	-	-	-	-
5	LANES	122,451,000.00	-	-	-	-
6	Ruzuku (Sekondari - Elimu Bila Malipo)	780,822,500.00	171,651,379.28	21.98%	171,651,379.28	100%
7	Ruzuku (Msingi - Elimu Bila Malipo)	1,137,975,537.98	306,873,460.69	40.05%	306,873,460.69	100%
8	Programme for Result - P4R	400,000,000.00	-	-	-	-
9	Mfuko wa Jimbo (CDCF)	55,646,000.00	-	-	-	-
10	Global Fund	9,385,000.00	9,261,159.33	98.68%	4,400,000.00	47.51%
11	UNICEF	10,000,000.00	-	-	-	-
12	Mtoto Mwelevu (IMA)	23,414,102.00	-	-	-	-
14	Management Development for Health – MDH	619,435,600.00	123,351,880.00	19.91%	122,579,753.00	99.37%
15	Mapato ya Ndani (40%)	582,619,200.00	100,066,884.81	17.18%	81,982,745.11	81.93%
16	Mfuko wa Hifedhi ya Jamii (TASAF III)	1,027,559,000.00	236,454,360.00	23.01%	236,343,000.00	99.95%
Jumla Ndogo Miradi ya Maendeleo		**6,949,711,750.98**	**947,659,124.11**	**13.64%**	**923,830,338.08**	**97.49%**

6.1 Fedha za Elimu Bure Sekondari – Tshs. 171,651,379.28

Mhe. Mkuu wa Mkoa;

Fedha hizi zimetumika katika kuwezesha utoaji wa Elimu bure kwa Shule za Sekondari 15 ambazo zinamilikiwa na Serikali.

6.2 Fedha za Elimu Bure Msingi – Tshs. 306,873,460.69

Mhe. Mkuu wa Mkoa;

Fedha hizi zimetumika katika kuwezesha utoaji wa Elimu bure kwa Shule za Msingi 80.

6.3 Fedha za Global Fund – Tshs. 4,400,000.00

Mhe. Mkuu wa Mkoa;

Fedha hizi zimetumika katika kutoa huduma na dawa kwa wagonjwa wa Kifua Kikuu Wilayani katika Ngazi za Kata, Mitaa, Vijiji na Vitongoji vyote kwa kupitia Vituo vya Tiba vilivyopo.

6.4 Fedha za MDH – Tshs. 122,579,753.00

Mhe. Mkuu wa Mkoa;

Fedha hizi zimetumika katika kutoa huduma, dawa kwa wagonjwa wa UKIMWI na kulipa mishahara kwa Watumishi wa MDH Wilayani katika Ngazi za Kata, Mitaa, Vijiji na Vitongoji vyote kwa kupitia Vituo vya Tiba vilivyopo.

6.5 Fedha za Mapato ya Ndani – Tshs. 81,982,745.11

Mhe. Mkuu wa Mkoa;

Fedha hizi zimetumika katika Ukamilishaji wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo na pia katika kutoa Mikopo katika Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Walemavu katika Ngazi za Kata, Mitaa, Vijiji na Vitongoji vyote. **(*Taarifa ya kina imeambatishwa katika Jedwali*)**

6.6 Fedha za TASA III – Tshs. 236,343,000.00

Mhe. Mkuu wa Mkoa;

Fedha hizi zimetumika katika kulipa Kaya Maskini, ambapo kiasi cha Tshs. 219,984,640 kilitumika kulipa Walengwa 2,965 na kiasi cha Tshs. 16,358,360.00 kilitumika katika kufanikisha zoezi hilo la malipo kwa kaya maskini na hivyo kufanya jumla ya matumizi kuwa Tshs. 236,343,000.00

7.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA FEDHA BAKAA ZILIZO VUKA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

Mhe. Mkuu wa Mkoa;

Hadi Mwaka wa Fedha 2019/2020 unakamilika, jumla ya **Tshs. 1,809,668,811.10** zilivuka mwaka na kuingia mwaka 2020/2021 kwa mchanganuo ufuatao kwenye jedwali Na. 06 hapa chini.

Jedwali Na 06: Muhtasari wa Fedha za Bakaa 2019/2020 kuishia 31 Oktoba, 2020

CHANZO	FEDHA TOLEWA	FEDHA TUMIKA	ASILIMIA
SRWSS - ELIMU MSINGI	175,768,504.80	139,003,031.40	79.08%
MABOMA YA NYUMBA ZA WALIMU – ELIMU MSINGI	50,000,000.00	36,944,000.00	73.89%
MFUKO WA MISITU TANZANIA (TaFF)	296,770,306.30	28,759,009.00	9.69%
SWASH-AFYA	272,830,000.00	175,330,000.00	64.26%
EP4R - ELIMU MSINGI	720,000,000.00	84118170	11.68%
EP4R - ELIMU SEKONGARI	294,300,000.00	14,354,290.00	4.88%
JUMLA	**1,809,668,811.10**	**478,508,500.40**	**26.44%**

Hadi kufikia tarehe 31/10/2020 Jumla ya **Tshs. 478,508,500.40** zimeshatumika sawa na asilimia **26.44**

(*Majedwali yenye Mchanganuo wa Matumizi ya Fedha hizi kwa kila Chanzo yameambatishwa*)

8.0 CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2020/2021

Mh. Mkuu wa Mkoa;

Zifuatazo ni baadhi ya changamoto ambazo Halmashauri ya Wilaya inakumbana nazo katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo yake mbalimbali

i. Upandaji wa bei za ununuzi wa Saruji na Vifaa vingine vya ujenzi upatikanaji wake ni tatizo. Wazabuni wengi hutoa huduma wetu wamepandisha gharama haraka.
ii. Changamoto ya upatikanaji wa Mafundi kutokana na kigezo cha Asilimia 10 ya gharama za vifaa hii imesababisha. Miradi mingi kutokupata mafundi kwa wakati na kusababisha mchakato wa zabuni za mafundi kurudishwa zaidi ya hata mara tatu.
iii. Kuletwa kwa ramani na B.O.Q kutoka kwenye Wizara/Wafadhi zinazotoa fedha. Hali hii inapelekea Mradi kusuasua katika ukamilishaji. Mfano Miradi ya SWASH na WASH.

iv. Baadhi ya Miradi kupewa fedha za utekelezaji mapema na maelekezo yake kuja kwa kuchelewa kutoka kwenye vyanzo vya Fedha hizo. Mfano Fedha za SWASHS zilizotolewa Januari 2020 na maelekezo pamoja na miongozo kutolewa mwezi mei 2020.
v. Miradi mingi inayoanzishwa na wananchi kuchelewa kukamilika kutokana na wingi wa miradi na michango mbalimbali kwenye eneo husika.
vi. Ukosefu wa Fedha za Ufuatiliaji wa Miradi ya Maendeleo.

9.0 MIKAKATI ILIYOWEKWA KWA AJILI YA KUTATUA CHANGAMOTO HIZI ILIKUHAKIKISHA MIRADI INAKAMILIKA KWA WAKATI

Mh. Mkuu wa Mkoa;

Zifuatazo ni baadhi ya Mikakati ambazo Halmashauri ya Wilaya imeweka kwa ajili ya kutatua/kukamiliana na changamoto hizo ilikuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa wakati;

i. Halmashauri imeanzisha utaratibu wa kununua vifaa kwa pamoja ambapo imeanza kuagiza SARUJI za maeneo yote yenye utekelezaji kutoka Kiwanda cha Dangote ambapo bado kuna changamoto ya uzalishaji Kiwandani.
ii. Changamoto ya upatikanaji wa Mafundi kwa kigezo cha asilimia 10 ya gharama ya vifaa, Halmashauri imefanya jitihada kila wakati kwa kufanya mazungumzo "Negotiation" na Mafundi ya malipo yao kwa vigezo vilivyowekwa. Lengo ni mafundi hao waweze kufanya kazi kutegemeana na mpango kazi uliowekwa japokuwa mwitikio toka kwa mafundi bado ni mdogo sana gharama hiyo ya asilimia 10 inahitaji kupanda kulingana na hali ya maisha kwa sasa.
iii. Kuhusu changamoto yakuletewa Ramani na B.O.Q toka kwenye vyanzo vya fedha, Halmashauri ya Wilaya imekuwa ikifanya mapitio ya michoro, Ramani, B.O.Q na kuwasilisha mapungufu yanayopatikana kwa mamalaka zinazotoa fedha hizo.
iv. Halmashauri ya Wilaya kuendelea kufanya mawasiliano na mamlaka zinazotoa fedha ilikupata Mwongozo wa matumizi moja kwa moja na kwa haraka.
v. Miradi viporo inayoanzishwa na nguvu za wananchi changamoto hii imewasilishwa OR-Tamisemi kipindi cha maandalizi ya Mipango na bajeti yam waka 2020/2021 japokuwa Miradi iliyopewa kipaumbele bado fedha yake haijaletwa.

vi. Suala la ukosefu wa fedha za ufuatiliaji, Halmashauri imewasilisha changamoto hii OR- Tamisemi ili mwongozo wa bajeti wa mwaka 2021/2022 uzingatie suala hili.

Mh. Mkuu wa Mkoa;
Naomba kuwasilisha,

(*Dionis M. Myinga*)
Mkurugenzi Mtendaji (W)
BUKOMBE